

Ni Nani Aliye Upande Wa Bwana?

(Who Is On The Lord's Side?)

Na

Ellis P. Forsman

Ni Nani Aliye Upande Wa Bwana?

(Who Is On The Lord's Side?)

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 17, 2011

Ni Nani Aliye Upande Wa Bwana?

Kut. 32:26

Kut. 32:26, “Ndipo Musa akasimama katika mlango wa marago, akasema mtu yeyote aliye upande wa BWANA na aje kwangu. Wana wa Lawi wote wakamkusanyikia.”

Tunachopaswa Kufanya Ili Tuwe Upande Wa Bwana

Tukatae dhambi

- Gal. 5:17-25, “Kwa sababu mwili hutamani ukishindana na Roho, na Roho kushindana na mwili; kwa maana hizi zimepingana, hata hamwezi kufanya mnayotaka. Lakini mkiongozwa na Roho hampopo chini ya sheria. Basi matendo ya mwili ni dhahiri ndiyo haya, uasherati, uchafu, ujisadi, , ibada ya sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, vivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, husuda, ulevi, ulafi na mambo yanayofanana na hayo, katika hayo nawaambia mapema kama nilivyokwisha kuwaambia, ya kwamba watu watendao mambo ya jinsi hiyo hawata urithi usfalme wa Mungu. Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uwumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi; juu ya mambo kama hayo hakuna sheria. Na hao walio wa Kristo Yesu wameulusubisha mwili paamoja na mawazo yake mabaya na tamaa zake. Tukiishi kwa Roho na tuenende kwa Roho.”
- 1 Pet. 2:11, “Wapenzi nauasihi kama wapitaji na wasafiri, ziepukeni tamaa za mwili zipingano na roho.”
- Rom. 6:6, “Mkijua neno hili ya kuwa utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena;”

Tii maagizo yote ya Mungu

- Yak. 2:10, “Maana mtu awaye yote atakayeishika sheria yote, ila akajikwaa katika neno moja, amekosa juu ya yote.”
- 1 Yoh. 3:15, “Kila amchukiaye ndugu yake ni muuaji: nanyi mnajua ya kuwa kila muruaji hana uzima wa milele ukikaa ndani yake.”

Tushike maungamo yetu ya imani

- Heb. 10:23, “Na mlishike sana ungamo la tumaini letu, lisigeuke maana yeye aliyeahidi ni mwaminifu;”
- Mat. 14:22-32, “Mara akawalazimisha wanafunzi wake wapande chomboni na kutangulia mbele yake kwenda ng’ambo, wakati yeye alipokuwa akiwaaga mkuutano. Naye alipokwisha kuwaaga makutano, alipanda mlimani faraghani, kwenda kuomba. Na kulipokuwa jioni alikuwako huko peke yake. Na kile chombo kimekwisha kufika katikati ya bahari, kinataabika sana na mawimbi; maana upopo ulikuwa na mbisho. Hata wakati wa zamu ya nne ya usiku Yesu akawaendea, akienda kwa miguu juu ya bahari. Wanafunzi walipomwona akienda juu ya bahari, wakafadhaika wakisema, ni kivuli; wakapiga yowe kwa hofu. Mara Yesu alinena, akawaambia jipeni moyo ni mimi msiogope. Petro akamjibu, akasema, Bwana ikiwa ni wewe niamuru nije kwako juu ya maji. Akasema, njoo. Petro akashuka chomboni akaenda kwa miguu juu ya maji, ili kumwendea Yesu. Lakini alipouona upopo, akaogopa, akaanza kuzama, akapiga yowe akisema, Bwana niokoe. Mara Yesu akanyoosha mkono wake, akamshika, akamwambia, ewe mwenye imani haba mbona uliona shaka? Nao walipopanda chomboni upopo ulikoma.”

Tutoe karama zetu zote kwa ajili ya huduma ya Kristo

Mat. 25:14-30, “Maana ni mfano wa mtu atakaye kusafiri, aliwaita watumuwa wake, akaweka kwao mali zake. Akampa mmoja talanta tano, na mmoja tanta mbili, na mmoja talanta moja; kila mtu kwa kadiri ya uwezo wake akasafiri. Mara yule aliyepokea talanta tano akaenda akafanya biashara nazo, akachuma faida talanta zingine tano. Vilevile na yule mwenye mbili, yeye naye akachuma nyingine mbili faida. Lakini yule aliyepokea moja alikwenda akaifukia chini, akificha fedha ya bwana wake. Baada ya siku nyingi akaja bwana wa watumuwa wale, akafanya hesabu nao. Akaja yule aliyepokea talanta tano, akaleta talanta nyingine tano, akisema Bwana uliweka kwangu talanta tano; tazama talanta nyingine tano nilizopata faida. Bwana wake akamwambia vema mtumwa mwema na mwaminifu; ulikuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi; ingia katika furaha ya bwana wako. Akaja na yule aliyepokea talanta mbili, akasema, Bwana uliweka kwangu talanta mbili; tazama talanta nyingine mbili nilizopata faida. Bwana wake akamwambia vema mtumwa mwema na mwaminifu; ulikuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi; ingia katika furaha ya bwana wako.

Akaja na yule aliyepokea talanta moja, akasema Bwana nalitambua ya kuwa weye u mtu mgumu, wavuna usipopanda, wakusanya usipotawanya; basi nikaogopa, nikaenda nikaificha talanta yako katika ardhi; tazama unayo iliyo yako. Bwana wake akajibu akamwambia, weye mtumwa mbaya na mlegevu ulijua ya kuwa navuna nisipopanda, nakusanya nisipotawanya; basi ilikupasa kuiweka fedha yangu kwa watoa riba; nami nikija ningalipata iliyo yangu na faida yake. Basi, mnyang'anyeni talanta hiyo, mpeni yule aliye nazo talanta kumi. Kwa maana kila mwenye kitu atapewa na kuongezewa tele; lakini asiye na kitu, hata kile alicho nacho atanyang'wanywa. Na mtumwa yule asiyefaa mtupeni mbali katika giza la nje; ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno.”

Kwa Nini Tunapaswa Kuwa Upande Wa Bwana

Ni upande wenye furaha wa maisha

Mit. 3:11-18, “*Mwanangu usidharau kuadhibiwa na BWANA, wala usione ni taabu kurudiwa naye. Kwa kuwa BWANA ampendae humrudi, kama vile baba mwanawe ampendavyo. Heri mtu yule aonaye hekima, na mtu yule apataye ufahamu. Maana biashara yake ni bora kuliko biashara ya fedha, na faida yake ni nydingi kuliko dhahabu safi. Yeye ana thamani kuliko marijani, wala vyote uitamanivyo havilingani naye. Ana wingi wa siku katika mkono wake wa kuume, utajiri na heshima katika mkono wake wa kushoto. Njia zake ni njia za kupendeza sana, na mapito yake yote ni amani. Yeye ni mti wa uzima kwao wamshikao sana; ana heri kila mtu ashikamanaye naye.*”

Unapata heshima zaidi

- Yoh. 12:26, “*Mtu akinitumikia na anifuate nami nilipo, ndipo mtumishi wangu atakapokuwapo. Tena mtu akinitumikia, Baba atamheshimu.*”
- Mat. 18:20, “*Yesu akamjibu, mimi nimesema na ulimwengu waziwazi; siku zote nalifundisha katika sinagogi na katika hekalu, wakusanyikapo Wayahudi wote; wala kwa siri mimi sikusema neno lolote.*”

Kama Yesu yuko hapa tunapo kusanyika, tunapaswa kuwa pale, pia.

Ni sehemu yenye usalama.

- 1 Pet. 3:13, “*Naye ni nani atakayewadhuru, mkiwa wenye juhudzi katika mema.*”

- Rom. 8:31, “*Basi tuseme nini juu ya hayo Mungu akiwapo upande wetu ni nani aliye juu yetu?*”

Huu Ni Ulimwengu Wa Kibiasara

Je inalipa?

- Rom. 8:18, “*Kwa maana nayahesababu mateso ya wakati huu wa sasa kuwa si kitu kama utukufu ule utakaofunuliwa kwetu.*”
- 1 Kor. 2:9, “*Lakini kama ilivyoandikwa, mambo ambayo jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia, wala hayakuuingia katika moyo wa mwanadamu, mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao.*”
- Mat. 16:26, “*Kwani atafaidiwa nini mtu akiupata ulimwengu wote, na kupata hasara ya nafsi yake? Au mtu atatoa nini badala ya nafsi yake?*”

Kurudi nyuma hakulipi.

Demas. 2 Tim. 4:10, “*Maana Dema aliniacha akiupenda ulimwengu huu wa sasa...*”

Ninyi ni nuru ya ulimwengu.

Mat. 5:14-16, “*Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji hauwezi kusitirika ukiwa juu yam lima. Wala watu hawawashi taa na kuiweka chini pishi, bali juu ya kiango; nayo yawaangaza wote waliomo nyumbani. Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni.*”

Tumia karama yako ambayo ilitajwa hapo awali.

Jionyeshe kuwa umekubaliwa na Bwana.

2 Tim. 2:15, “*Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli.*”

Je Umejitoa Kwa Ajili Ya Yesu?

Ni utumishi wa maisha.

Wanajeshi wamepangiwa idadi ya miaka ya kufanya kazi ya kuitumikia nchi yao. Hawawezi kuicha kazi yao ambayo wamepewa. AWOL (Hayupo Bila Likizo) – kufungwa.

Ufu. 2:10, “*Usiogope mambo yatakayokupata; tazama huyo ibilisi atawatupa baadhi yenu gerezani ili mjaribiwe, nanyi mtakuwa na dhiki siku kumi. Uwe mwaminifu hata kufa, nami nitakupa taji ya uzima.*”

AWOL katika huduma kwa Yesu – adhabu ya milele.

- 2 Pet. 2:19-22, “*Wakiwaahidia uhuru nao wenyewe ni watumwa wa uharibifu, maana mtu akishindwa na mtu huwa mtumwa wa mtu yule. Kwa maana wale waliokwisha kuyakimbia machafu ya dunia kwa kumjua Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo, kama wakinaswa tena na kushindwa, hali yao ya mwisho imekuwa mbaya kuliko ile ya kwanza. Maana ni heri wasingalijua njia ya haki, kuliko kujua kisha kuiacha ile amri takatifu waliopewa. Lakini imetukia kwao sawasawa na ile mithali ya kweli, mbwa ameyarudia matapiko yake mwenyewe, na nguruwe aliyeoshwa amerudi kugaagaa matopeni.*”
- Ufu. 21:8, “*Bali waoga na wasioamini, na wachukizao, na wauaji, na wazinzi, na wachawi, na hao waabuduo sanamu, na waongo wote, sehemu yao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya pili.*”

Jinsi Ya Kufanyika Mkristo

Tii kutoka moyoni.

Rom. 6:17, “*Lakini Mungu na ashukuriwe kwa maana mlikuwa watumwa wa dhambi, lakini mliitii kwa mioyo yenu ile namna ya elimu ambayo mliwekwa chini yake,*”

Amini.

Heb. 11:6, “*Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao.*”

Tubu.

- Mdo. 2:38, “*Petro akawaambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*”
- Luka 13:3, “*Nawaambia sivyo, lakini msipotubu, ninyi nyote mtaangamia vivyo hivyo.*”

Kiri.

Rom. 10:9, “*Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka.*”

Mat. 10:32, “*Basi kila mtu atakayenikiri mbele ya watu, nami nitamkiri mbele ya Baba yangu aliye mbinguni.*”

Ubatizwe.

- Gal. 3:27, “*Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo.*”
- Mdo. 2:38, “*Petro akawaambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*”
- 1 Pet. 3:21, “*Mfano wa mambo hayo ni ubatizo, unaowaokoa nanyi pia siku hizi: sio kuweka mbali uchafu wa mwili, bali jibu la dhamiri safi mbele za Mungu, kwa kufufuka kwake Yesu Kristo.*”

